



Seti ya Shughuli za Michezo



AGA KHAN FOUNDATION
An agency of the Aga Khan Development Network



UTANGULIZI

Mojawapo ya njia bora za kusaidia ukuaji wa mtoto ni rahisi na ya kufurahisha. Kucheza kunaweza kuonekana kana kwamba kunahusu kujifurahisha tu, lakini ni zaidi ya hiyo kwa watoto. Kunahusu kusoma na kustawisha stadi muhimu za maisha ikiwa ni pamoja na kueleza mawazo na kutatua matatizo.

Baada ya kusikiliza hadithi, unaweza

1. Ambia mtoto aeleze mhusika au sehemu ya hadithi anayoipenda (Angalia mchezo fumbo wa kupanga vipande ili kupata picha kamili au Sehemu za hadithi). Mtoto anapofikiria na kuchora mwenyewe, anastawisha ustadi wa ubunifu.
2. Waambie watoto waigize hadithi (Angalia Vifaa vya Hadithi au Kuiigiza). Mtoto anapoigiza, kucheza au kuimba, anastawisha ustadi wa kihisia.
3. Mwambie mtoto atengeneze ndege (chombo cha usafiri)/ndege (kiumbe anayeruka angani) kwa kutumia karatasi, ngoma au gari (Angalia Kukunja na kupaa, Gari la kucheza lililorejelezwa, au ngoma ya Nazi). Mtoto anapotengeneza, anafanya mazoezi ya ustadi wa kimwili.
4. Waambie watoto warekodi hadithi kwenye Tengeneza kadi yako mwenyewe (Angalia Kurekodi mwongozo wa hadithi yangu mwenyewe), Jaribu kadi ya Toa Sauti hiyo, waulize watoto inatoa sauti gani? Mtoto anapotoa sauti za kipuuzi, anastawisha ustadi wa kijamii.
5. Acha watoto waunde na wacheze michezo kutokana na hadithi. (Angalia Unda mchezo wako wa ubao) Watoto wanapocheza michezo, wanastawisha ustadi wa kimantiki.
6. Waulize watoto maswali kuhusu hadithi hiyo. Je, ni sehemu gani za hadithi walizopenda zaidi? Ilikuwa ya kuchekesha?

Ifuatayo ni mifano ya maswali ambayo unaweza kuuliza kwa hadithi za Kabrazen

- *Ni jambo gani ambalo Mekatilli alipenda kufanya zaidi? (kucheza, kukimbia, kucheza dansi, kuimba)*
- *Mekatilli alizaliwa wapi (Malindi, Kilifi, Mombasa, Taita Taveta)*
- *Ni msichana gani ambaye angweza kufungua fundo lolote? (Mekatilili, Fatima, Maryam, Njinga)*
- *Fatima na Maryam walizaliwa katika nchi gani?*
- *Chuo Kikuu walichojenga kinaitwaje?*
- *Je, Fatima na Maryamu wanalingana kwa njia gani?*
- *Je, msichana mtulivu alijifunza nini kutoka kwa udongo?*
- *Je, msichana mtulivu aligundua nini kuhusu mtu wa jiwe?*


Watoto hawahitaji vifaa vingi vya kucheza na kusoma. Labda una vifaa unavyohitaji kwa shughuli za kujifurahisha. Utahitaji karatasi na vitu vingine kama vile chupa za maji zilizorejelezwa au nazi. Nyuma ya kifurushi hiki, utaona violezo ambavyo unaweza kutumia katika shughuli hizi.

SHUGHULI Kuiigiza

Nyenko zinazohitajika:

1. Kadi za maneno zilizokatwa kutoka kwa kiolezo
2. Kadi tupu za kuongeza maneno

MAELEKEZO:




1. Mtoto mmoja achukue kadi na asionyeshe mtu mwingine yeyote.

2. Mtoto huyu ajaribu kuwafanya wengine kukisia neno lililo kwenye kadi kwa kuigiza neno lililo kwenye kadi na kutumia miondoko ya miili yao. Mtoto lazima ajaribu kufanya hivyo bila kuongea.



3. Wacha kila mmoja
aweze kuchagua kadi
kwa zamu.



MATOKEO YA MWISHO

Kiendelezi

Tengeneza orodha yako mwenyewe ya vitu na watu wanaoweza kuigizwa katika hadithi. Andika kila kipengele katika karatasi.

- | | |
|--------------|--|
| A. Jahazi | G. Ndege |
| B. tuk tuk | H. Uvubi |
| C. boda boda | I. Ngoma |
| D. Punda | J. Kucheza dansi |
| E. Simba | K. Kandanda |
| F. Ndovu | L. Msanii maarufu wa muziki afrika mashariki |

SHUGHULI

Gari la kuchezza lililorejelezwa

Nyenko:

1. Chupa ya plastiki
2. Vifuniko 4 vya chupa
3. Vijiti 2 vya mbao
4. Kisuu au kitu cha kukata vijiti
5. Kamba

MAELEKEZO:



1. Safisha chupa ya plastiki



2. Kata mashimo mawili katika kila upande wa chupa




3. Weka vijiti kupitia kwa mashimo


4. Toboa shimo ndogo katika kila kifuniko cha chupa na uziambatishe kwenye vijiti




5. Kata kidogo sehemu ya juu ya chupa baada ya kuweka magurudumu (ili kuwa nafasi ya viti au kubeba vitu)



6. Funga kamba katika sehemu ya juu ya chupa



7. Livute gari kwa kutumia kamba



Kiendelezi

Fanya mazoezi ya kuvuta gari kutoka mahali pa kuanzia hadi mwisho kwa njia ya moja kwa moja, kwa kulipindapinda kulizungusha katika mduara, chini ya meza, juu ya kilima bandia, na kadhalika.

Toa maagizo mtoto anapolivuta gari (kwa mfano., nenda moja kwa moja, kulia, kushoto, rudi nyuma)

SHUGHULI

Vifaa vya Hadithi

Nyenko zinazohitajika:


1. Karatasi au kadibodi
2. kiolezo cha barakoa
3. Krayoni, penseli za rangi au kalamu za kuweka alama

MAELEKEZO:


Kundi 1



Kundi 2



1. Waweke watoto
katika vikundi ili
watengeneze vifaa



2. Tengeneza
vifaa tofauti vya
watu au
wanyama
kulingana na
hadithi

MATOKEO YA MWISHO



A. Chura wa Kabrazen kutoka
Hadithi ya Mekatilili



3. Acha kila kikundi
kiigize hadithi kwa
kutumia vifaa vyao



4. Hifadhi rasilimali ili
kuweza kuzitumia siku
zijazo kusimulia hadithi



B. Kinyago cha Magury kutoka
kwenye hadithi ya maguro


Kiendelezi

Waambie watoto watengeneze vifaa kwa kutumia nyenzo zilizorejelezwa au za zamani walizonazo nyumbani. Kwa mfano, chupa ya plastiki inayoweza kurejelezwa inaweza kutumika kutengeneza mhusika wa chupa ya plastiki (inaweza kujazwa mawe au udongo ili kutoa sauti). Nguo ya zamani au kanga inaweza kutumika kutengeneza kikaragosi cha mkono au juba.

SHUGHULI

Ngoma ya Nazi

MAELEKEZO:



1. Hakikisha nazi imekatwa katikati- mtu mzima akusaidie



2. Safisha nazi na uhakikishe kuwa hakuna vipande vyeupe vilivyobaki ndani



3. Kata mfuko wa plastiki katika duara kubwa, kubwa kuliko nazi



4. Sasa tandaza plastiki kwenye nazi na kuifunga kwa kamba au ukanda wa mpira



5. Jaribu kutengeneza ngoma kwa vifaa vingine, unaweza kurudia mchakato huo kwa kutumia nguo badala ya plastiki. Unaweza pia kutumia mikebe ya bati badala ya nazi. Ni nyenzo gani zinazotoa sauti kubwa zaidi?



MATOKEO YA MWISHO

Kiendelezi


- Chezeni midundo kwa zamu kwa kugonga ngoma
- Nakili mdundo wa kila mmoja kwa zamu
- Gusa mpigo- punguza kasi, iharakishe, ifanye kuwa na sauti kubwa zaidi, ifanye iwe tulivu zaidi
- Cheza kwa kufuata mpigo au mdundo

SHUGHULI Sehemu za hadithi

Nyenko:

1. Karatasi nyeupe
2. Penseli, penseli za rangi au krayoni


MAELEKEZO:




1. Gawanya karatasi katika sehemu tatu kwa kuikunja

Mwanzo	Kati	Mwisho


2. Weka alama kwenye sehemu tatu, mwanzo, kati na mwisho



4. Waambie watoto
wachore kilichotokea
katikati ya hadithi



3. Waambie watoto
wachore kilichotokea
mwanzoni mwa hadithi



5. Waambie watoto
wachore kile
kilichotokea mwishoni
mwa hadithi



Kiendelezi


Acha mtoto achore na asimulie
hadithi ya kilichotokea katika siku
maalum (kwa mfano sikukuu ya
Kenya au siku ya kuzaliwa)

MATOKEO YA MWISHO


SHUGHULI

Kukunja na kupaa


MAELEKEZO:




1. Kunja karatasi
katikati



2. Kunja pembe za
juu zikielekea
upande wa chini




3. Kunja ncha za
nje zikielekea
ndani tena




4. Sasa kunja karatasi
katikati ukifuata ya mstari
wa katikati

Nyenko:

1. Karatasi ya A4
2. Penseli za rangi au krayoni




5. Kunja mabawa kuelekea juu, yanapaswa kukutana na sehemu ya chini ya ndege



6. Inua mabawa juu na ndege yako iko tayari kupaa



7. Chora kwenye ndege za karatasi kwa kutumia penseli za rangi, alama au krayoni penseli za rangi kalamu za kuweka alama au krayoni



8. Sogea mahali palipo wazi na ujaribu kuipaisha ndege. Ni ndege gani inapaa juu zaidi?



Kiendelezi

Weka lengo (kwa mfano mti) na ujaribu kuona ni nani anayeweza kuipaisha ndege yake karibu na mti

MATOKEO YA MWISHO

SHUGHULI

Mchezo fumbo wa kupanga vipande ili kupata picha kamili

MAELEKEZO:



1. Chora sehemu unayoipenda ya hadithi na mhusika unayempenda katika karatasi kubwa. Picha inapaswa kutumia nafasi kubwa ya karatasi iwezekanavyo. Ikiwa mtoto ni mdogo unaweza kutumia kiolezo.

Nyenko:


1. Karatasi au kadibodi
2. Kalamu za rangi za kuweka alama
3. Mkasi




2. Paka rangi picha ya mhusika unayempenda



3. Kata vipande katika vipande kadhaa vyaa mafumbo, vipande hivi vinaweza kuwa maumbo ya kawaida kama vile mistatili au pembetatu.



4. Changanya vipande hivyo katika mfuko



5. Badilishana fumbo lako na rafiki. Kila mtoto anapaswa kukamilisha fumbo ili kutengeneza upya picha asili iliyochorwa na rafiki yake. Ikiwa unatumia kiolezo cha mafumbo basi utakuwa ukipanga vipande ili kuunda mtu



MATOKEO YA MWISHO

WORDS	
I H F P T G R A S S	1. HARE
J F A R R A C E X U	2. TORTOISE
E X T H A P D M P N	3. RACE
L L O S T A R N X Q	4. FINISH LINE
F I N I S H L I N E	5. START
L A N G L A E O D T	6. NAP
K N N R O R A G S E	7. WIN
F I S ! W E F A S T	8. LOST
	9. SLOW
	10. FAST
	11. SAD
	12. PRIDE
	13. HAPPY
	14. LONG
	15. GRASS
	16. TREE
	17. GATE
	18. FAR

Kiendelezi

Tengeneza fumbo la kujaza maneno kulingana na maneno yaliyotumika katika hadithi



SHUGHULI

Unda mchezo wako mwenyewe


Nyenko:

- Penseli za rangi au kalamu za kuweka alama
- Vifuniko vya chupa (kama vipande vya mchezo wa ubao)
- Kete kutoka kwa kiolezo

MAELEKEZO:




- Chagua mtindo wa mchezo kutoka kwa mojawapo ya violezo vilivyoambatishwa



- Pamba mchezo wako wa ubao na wahusika kutoka kwenye hadithi

MATOKEO YA MWISHO




3. Tengeneza kete kutoka kwa kiolezo



4. Unda sheria za mchezo wako
5. Cheza mchezo wako na kikundi

Kiendelezi



Herufi Zinazosimulia Hadithi- Sambaza kadi za alfabeti na uziweke zikielekea chini. Watoto watachagua kadi moja ya herufi bila mpangilio maalum. Kisha wataunda hadithi inayohusiana na herufi hiyo (kwa mfano M inaweza kuwakilisha madafu). Watoto wacheze kwa zamu.

Tafuta Vifaa- Bandika kadi ya herufi kwenye kifaa (kwa mfano S ni ya kitabu cha katuni cha Shujaaz). Kisha waulize watoto kutafuta katika na karibu na maktaba kifaa kinachoanza kwa herufi S.


SETI YA SHUGHULI ZA VIOLEZO

>>

TUK TUK




NGOMA



NDEGE



UVUVI



JAHAZI



BODA BODA




INSTRUCTIONS

Cut on the dotted line & use the cards for
Activity 2: Act It Out

NDOWU



PUNDA



**MSANII MAARUFU WA
MUZIKI AFRIKA
MASHARIKI**



Diamond Platnumz

SIMBA



KANDANDA





**KUCHEZA
DANSI**




INSTRUCTIONS


Cut on the dotted line & use the cards for
Activity 2: Act It Out

























Ee




Jj




Dd



Ii



Cc




Hh




Bb




Gg



Aa




Ff




Oo




Tt




Nn




Ss



Mm




Rr




Ll




Qq




Kk



Pp



Yy



Xx



Ww



Vv



Uu



Zz

PLAYKIT ACTIVITIES



AGA KHAN FOUNDATION
An agency of the Aga Khan Development Network

PLAYKIT

ACTIVITIES

TEMPLATES